By Leonard .F. Mushumbusi
Ilboru high school
@2018

# Asante kwa yote






2. Umenilisha kwa mwili wako,nakushukuru Baba.
Umeninywesha kwa damu yako,nakushukuru Baba,
Vingi vipaji vya tofauti,unanikirimia,
Nitoe shukrani gani Mimi,Kulipa wema wako.

3.Leo kati yao ndugu zangu ,nakutangaza wewe.
kwa talanta yangu uimbaji,ninakusifu wewe'
Nakupa maisha yangu mimi,uyatawale wewe
Mimi kwako ni kiumbe duni ,nitegemeze Bwana

4.Shukrani toka moyoni mwangu,Naelekeza kwako,
Ajali pia maradhi mengi,waniepusha mimi,
Sina neno zuri kwa shukrani,Asante Mungu wangu,
Pokea sifa toka moyoni.Uhimidiwe wewe.

5.Na kwa mataifa hayo yote ,nitakutaja wewe,
Nitalitangaza Jina lako,tukuhimidi wewe,
Nitawakumbusha wenye mali,wakufuase wewe
kwani hizo ni neema zako wawatiririshia.

6.Tazama wanyama na mimea ,ulivyoumba wewe,
Dunia nayo uloijaza,kwa watoto wazuri,
Ona wanadamu tunangara kwa sura yako wewe
kwa shangwe nayo furaha kubwa tunarudisha sifa

lennyflorence@gmail.com
0626574894